# *Ushawishi*

Asante, sana. Hebu tuendelee kusimama kwa muda mfupi tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi. Na tunapoinamisha vichwa vyetu, na mioyo yetu, nashangaa ni wangapi walio na haja, wangeifanya ijulikane kwa Mungu mnapoinua mikono yenu? Na sasa shikilieni haja zenu tunapoomba.

2 Baba uliye Mbinguni, tuna furaha sana usiku wa leo kwa huu, wakati mwingine tunapoweza kuja Kwako, na kuwa na matumaini ya kwamba tunachoomba tutapokea, tukiamini ya kwamba tutapata tulichoomba. Na sasa, Bwana, tusaidie kutokuamini kwetu, kusudi usiku wa leo tupate kupokea mambo haya ambayo tumeyaomba. Mikono yangu, pamoja na mikono yao, imeinuliwa. Nasi tunaomba, Baba, Kwako Wewe unayefahamu mambo tunayohitaji. Tujalie, hayo, sisi, Bwana, usiku wa leo. Tunaomba tupate kutiwa moyo, ili kwamba tunapokuwa katika majira haya ya shida nyingi tunayoishi, u . . . na ulimwengu ukiwa katika hall uliomo, tunahitaji usaidizi Wako ulio Mtakatifu sana, Bwana. Na tunaomba ya kwamba utatutia moyo kwa Neno Lako, tupate kujua itupasavyo kutenda, kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana Yesu. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

3 Nafurahia sana kurudi tena usiku wa leo, na kuzungumza tena usiku wa leo juu ya Bwana wetu mwenye neema nyingi. Ni vizuri kurudi humu Lane Tech tena. Hii ni kama tu kuja nyumbani; nimekuwa hapa mara nyingi sana. Na sasa naona ya kwamba wana leso nyingi sana hapa ambazo zimewekwa hapa kuombewa. Na sasa, usiku uliopita, ilitulazimu, tulikomesha ibada yetu ya kawaida ya uponyaji, tukachukua kadi na kadhalika, kwa sababu ya kuwa na ibada maradufu. Unaona, inakuchosha, kuwa na ibada ma—maradufu. Na sasa bila shaka, tutaombea leso hizi usiku wa leo, tukitumainia ya kwamba Bwana atamfanya kila mmoja wenu, kuwa na imani hata mtapokea mliyoomba katika maombi haya.

4 Bila shaka tutamkosa Ndugu Mel Johnson kesho, na huko kuimba kuzuri. Bila shaka nafurahia hiyo sauti nzuri ambayo Bwana amempa.

5 Na sasa, kesho, iwapo wewe ni mgeni hapa, nitawaambia watu wa Maskani, kuna . . . nina marafiki hapa kutoka Jeffersonville. Nafikiri kwenye kanisa la Philadelphia, Ndugu Mead, ndugu yetu, nafikiri wana ibada kule. Nami sijui kama ninyi, ninyi mna ibada? Kuna ibada. Wewe, saa ngapi? [Mtu fulani asema, "Tano."] Saa tano, kutakuwa na ibada kule. Na

nakisia nitarudi yapata saa saba u nusu, ama nane, yapata . . . Tisa, ni—nitakuweko saa tisa, saa tisa, na—na saa moja tena kesho jioni. Kwa hivyo bila shaka tunataka kuwaalika kwa furaha ninyi nyote kuja kwenye ibada, iwapo hamna ibada kanisani mwenu.

6 Bila shaka hatungetaka kuwaondoa kutoka kwenye wajibu wenu, kwa sababu hiyo siyo shabaha yetu. Ni kujaribu kuwapata, hasa, wale ambao hawajaokolewa. Wale ambao hawana Roho Mtakatifu, nanyi—nanyi bila shaka mwaamini ya kwamba mnamhitaji, ndiposa tuko hapa kuwasaidieni. Kisha walio wagonjwa na wanaoteseka, naam, tuko hapa kuwaombea, kutoka makanisani mwote. Nanyi mrudi kanisani mwenu, po pote mlipotoka. Iwapo ulimpokea Roho Mtakatifu, ama ukaponywa, rudi ukiwa na ushuhuda, waambie wengine. Hata ingawa kanisa lako haliamini, nenda kwa vyo vyote. Unaona? Ambapo, ni rahisi kuangaza Nuru yako ambapo mna Nu—Nuru nyingi, bali tunataka Nuru iangaze ambapo hamna Nuru. Hapo ndipo inatoa ushawishi wake ulio bora sana.

7 Na asante Ndugu Vayle [Ndugu Vayle alikuwa ametengeneza maikrofoni, na sasa anasema "Ikae *hivi* hata hatuna budi kuiangalia."—Mh.] Ndugu Vayle alikuwa akifikiri hawangalisikia. Hiyo ni bora? Vema, vizuri hivyo ni vyema.

8 Sasa, usiku wa leo, bila ibada ya uponyaji, nafikiri, yanipasa nitoke mapema kidogo usiku wa leo. Ni—nimekuwa nikisema, kila usiku, "Nitajaribu kuwaachilia muondoke yapata saa tatu u nusu." Na imekaribia sana wakati huo sasa, na kwa hivyo, saa tatu, na kama dakika tano hivi. Basi ni wakati wa kumaliza, halafu naliwachelewesha asubuhi hii yapata masaa mawili, nitawaambia, labda mtakuwa mmechoka sana na mtafurahia nitakapoondoka mjini kesho usiku. Lakini napenda ningalijishusha kwenye yale mazungumzo ya dakika ishirini na tano. Bali inanibidi tu kuendelea kuzungumza hata nitakapochoka, nami najua mmechoka sana wakati huo. Kwa hivyo basi mimi sipati kumaliza; naondoka tu na kuingia ndani, na kupumzika kidogo.

9 Basi usiku wa leo, nawatakeni mfungue kwenye Biblia zenu, katika Isaya, Kitabu cha Isaya, su—sura ya 6 ya Isaya. Na sasa kabla hatujasoma, tutamuuliza Mungu abariki Neno Lake na—na kulifanya halisi kwetu, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi. Vema, tutalisoma Neno kwanza, basi sikizeni kwa makini tunapolisoma.

> *Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia* nilikuwa . . . *nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.*

*Juu yake walisimana maserafi; kila mmoja alikuwa ma mabawa sita, kwa mawili alifunika uso wake na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.*

*Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni* BWANA *wa majeshi, dunia yote imejaa utukufu wake.*

*Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.*

*Ndipo niliposema, Ole wangu! kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme,* BWANA *wa majeshi.*

*Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;*

*Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.*

*Kisha nikasikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume Mimi.*

10 Natuombe. Bwana Yesu, sisi hatufai kufungua fungu hili la maneno yenye neema sana, usiku huu, bali tunaomba msaada Wako sasa, Bwana, si kwa kusudi lingine bali kwamba I—Injili ipate kuhubiriwa tena katika Jiji la Chicago. Tujalie, Bwana. Na u—ushawishi na uwe ushawishi wa milele. Tujalie. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

11 Sasa nataka kuchukua fungu la maneno kutoka kwa haya, la: *Ushawishi*. Wajua, kuna jambo au jingine sisi tulilo, sisi, tutendavyo, tunamshawishi mtu mwingine kwa yale tutendayo, jinsi tutendavyo, jinsi tunenavyo, jinsi tunavyoishi. Na yote tutendayo, tunamshawishi mtu mwingine.

12 Na sasa, mwajua, watu wengi hawataenda kanisani. Wao husema. . . Vema, wao wana fikara mbaya kuhusu kanisa. Wanafikiri wa—wanawake kule ni—ni wachawi, na—nao wanaume ni pepo waliovalia majoho meusi, nao wamepata tu mawazo mabaya kuhusu hayo. Lakini nitakwambia wafanyavyo, watayaangalia maisha yako kuona ufanyavyo. Naamini ilikuwa Paulo aliyesema "Sisi ni barua zilizoandikwa za Mungu, zinazosomwa na watu wote." Unapokuwa barabarani, unapokuwa kazini mwako, na popote ulipo, mtu fulani yu akutazama.

13 Na zaidi sana baada ya kusema na kukiri ya kwamba wewe ni Mkristo, wao watakuchunguza kwa makini zaidi, na hilo hutoa ushawishi kwa—kwa watu walio karibu nawe. Na

inatubidi kuchunguza tunayofanya. Kwa maana, kama tukitoa ushawishi mbaya, basi tunasababisha shutuma, si sana kwetu sisi, bali juu ya yale tunayodai kuwa, Wakristo, tunaileta juu ya Kristo. Na hamna ye yote, ikiwa tungaliwazia, hangalitaka kuleta shutuma juu ya Kristo. Bali tendo baya, wakati usiofaa, bila shaka litasababisha sifa baya kwa mtu anayekutazama. Na kila mtu huchunguzwa, unapokiri kuwa Mkristo.

14 Sasa fungu hili la maneno tunalozungumzia usiku wa leo, juu ya ushawishi, linarudi nyuma, somo lake halisi, iwapo ungetaka ku—kusoma, utalipata katika kitabu cha Pili cha Mambo ya Nyakati, sura ya 26. Ilikuwa maisha ya huyu Uzia, mfalme.

15 Basi, mfalme Uzia alikuwa mvulana mchungaji. Yeye alikuwa kijana, ambaye ni mwana wa mfalme, naye alipenda kuwa nje. Ye—yeye alipenda mwi—mwitu na alikuwa mchungaji. Pia alipenda shamba la mizabibu, yeye alipenda kuona vitu vikikua. Naye huyu kijana alikuzwa chini ya ushawishi mzuri. Amazia, babaye, alikuwa mtu mashuhuri katika siku zake, za mwisho yeye alilegea kidogo, na kutwaa baadhi ya miungu kutoka nchi nyingine, naye Bwana basi akamwondoa duniani. Bali kijana huyu alikuwa ameishapata ushawishi mzuri, kwa maana mamaye alikuwa binti wa Yerusalemu, babaye mwamini, na kwa hivyo huyu ki—kijana alipata malezi yenye ushawishi mzuri.

16 Na hiyo ni njia nzuri ya kumlea mtoto, katika njia impasayo. Nawe wajua nini? Watoto wako ndio moja ya macho muhimu yanayokuangalia. Wao wanaangalia utendayo. Na cho chote ufanyacho, wao wanakuigiza, kwa maana wewe unawaonyesha mfano mbele yao, jinsi utendavyo.

17 Inanikumbusha. Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa kwenye mkutano wa Wafanyi Biashara wa Injili Yote, kule Los Angeles. Naye Ndugu Oral Roberts alikuwa amefanya matamshi kuhusu jambo hili, nao wakaniomba nisimame na kusema neno juu yake, juu ya kushawishi. Nalisema:

18 Inanikubusha juu ya hadithi moja niliyosoma wakati mmoja, ambapo m—mtu fulani aliondoka akaenda zake, siku inayotangulia Krismasi, akipeleka zawadi kijijini, kwa wenziwe, majirani. Na kila wakati, alipoenda mahali po pote, ye—yeye akanywa pombe. Angeingia kwenye nyumba ifuatayo, angekunywa pombe. Na wakati alipokuwa amekwisha toa za—zawadi zake zote na zile alikuwa amekusanya; alipokuwa njiani akirudi, akafikiri angechukua njia ya mkato kupitia bustanini. Nayo theluji ilikuwa imeanguka yapata inchi nne ama sita. Naye akaona ya kwamba hangaliweza kutembea moja kwa moja, angeenda kwa kulegalegea kwa sababu alikuwa amelewa kwa vinywaji hivyo.

19 Basi akaona, huku nyuma yake, akija bila kuweza kufuatana naye, mtoto wake mdogo sana wa kiume, mwenye umri wa miaka saba; naye alikuwa akipiga hatua kubwa, huku akianguka, na kwenda akilegalegea. Kwa hivyo akangoja hata yule mvulana mdogo alipomfikia, naye akasema, "Mbona unatembea hivyo, mwanangu.?"

Akasema, "Baba, ninajaribu kufuatisha nyayo zako."

20 Mwaona ya kwamba hiyo ni zaidi ya—ya mfano, kwa sababu ni kweli, kwamba, watoto wako, unawafanyia kielelezo.

21 Na iwapo watu wetu wa Amerika wanafanya vielelezo leo, mbele ya watoto wetu, za kuvuta sigara, wanawake kwa wanaume, kunywa pombe, na karata nyumbani, na—na kucheza dadu, ni wa—watu aina gani tutakuwa nao katika taifa lijalo, au namaanisha katika kizazi kifuatacho. Litakuwa kundi la wasioweza kujizuia. Ambapo nafikiri ulimwengu mzima umo karibu kufikia hali kama hiyo sasa. Basi ikiwa taifa hili la watu, ama kizazi hiki, tuseme, kiko hivi, je, kifuatacho kitazaa nini? Kisha iwapo kungekuwa na kingine, naam, jamii yote ya binadamu, kama ikiendelea kuwa kama ilivyo, itaangamia, kabisa, kwa sababu tunajiva na kuwa vielelezo kwa wengine.

22 Na hata Wakristo siku hizi, wanaodai kuwa Wakristo, na wanavuta sigara na kunywa pombe, na—na kudanganya, na kununua kimagendo. Huku nasi. . .Naam, si ajabu ya kwamba Ukristo umefikia mojawapo wa viwango vyake vya chini sana wakati huu. Ni ushawishi ambao watu wa kanisa wame—wameuweka juu ya watu ambao bado hawajampokea Kristo. Watu wanataka kushikilia ushuhuda wao na kuishi watakavyo.

23 Basi hiyo ndiyo mojawapo ya sababu kwamba Roho Mtakatifu ni mu—mu—muhimu sana leo, kwa sababu ndiye anayeishi maisha yako. Huyaishi wewe mwenyewe. Ni Kristo ndani yako, basi, baada ya wewe kupokea Roho Mtakatifu. Na, na iwapo Yeye hana uongozi maishani mwako, basi wewe kumbuka tu, hujampokea Roho Mtakatifu. Maana, kama yuko ndani yako, Yeye ataishi maisha Yake Mwenyewe. Wewe si mali yako mwenyewe tena. "Ulikufa, na uhai wako ukafichwa pamoja na Kristo, katika Mungu, na mkatiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu." Kwa hivyo hamna njia kamwe kwako kuwa wewe mwenyewe tena, jinsi ulivyokuwa.

24 Sasa, huyu kijana, tunaona, yeye, akisha kukuzwa na hawa wazazi wazuri wacha Mungu na mafundisho, ili. . .Babaye alipokufa, naam, yeye alikuwa na miaka kumi na sita tu, nao watu wakamchukua wakamfanya mfalme. Naye akaja kwenye kiti cha enzi alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita tu. Na kama utasoma juu ya maisha yake, yeye hakushawishiwa na siasa za nchi yake. Ye—yeye hakukubaliana na maoni yanayopendwa. "Alimtafuta Mungu," Biblia ilisema.

25 Basi, hiyo, hiyo ndiyo ilimfanya kuwa kielelezo kikubwa kwa huyu nabii kijana, wakati uo huo, Isaya. Nabii Isaya aliishi katika siku za mfalme Uzia. Na wote wawili wakiwa vijana pamoja, nabii pamoja na mfalme, walikuwa marafiki wakuu. Naye Isaya aliishi katika jumba la kifalme, naye akaengemea mkono wa—wa mfalme. Nasi twaona ya kwamba ushawishi wa huyu kijana ulimshawishi Isaya. Yeye akawa shujaa kwa—kwa Isaya, kwa maana (yeye alikuwa) yeye hakuwatofautisha watu, hakuacha cho chote kimsukasuke huku na huko, naye aliamua kumtumikia Mungu, na kumtumikia Mungu peke Yake. Na huyo ni mtu mzuri kuchukua mfano wake. Yule . . .

26 Nasi twaona ya kwamba yeye hakupatana na ulimwengu wa kikafiri kamwe, ulimwengu wa kikafiri; baada ya kumwona yeye akistawisha ufalme wake kuwa mkubwa sana, na Mungu alikuwa pamoja naye na akimbariki.

27 Na Mungu atambariki mtu ye yote atakayedumu na Neno Lake. Sasa, hiyo ni, ni wajibu wa Mungu kufanya hivyo, kumbariki mtu ye yote ambaye atadumu na Neno la Mungu.

Nasi twaona ya kwamba Isaya bila shaka alimpenda huyu mfalme.

28 Kisha ufalme wa huyu mfalme ukaenea. Nakisia alikuwa wa pili kutoka kwa Suleimani, katika ufalme wake, kwa sababu enzi yake ilifika hata Misri.

29 Ulikuwa msaada mkubwa sana kwa Isaya, huyo nabii kijana, kuona ya kwamba mtu ye yote atakayesimama na Mungu, na bila kufikiria siasa ama cho chote kile, atadumu kabisa na Neno. Bila shaka ilimshawishi nabii, Isaya. Huyu kijana, jinsi Mungu alivyombariki, kwa sababu alilitii Neno.

30 Sasa tunaona ya kwamba huyu mfalme, lo, alitenda kama Wakristo wengi wa siku hizi. Mradi tu alidumu akiwa mnyenyekevu, basi Mungu alimbariki. Bali Biblia ilisema hapa, ya kwamba, "Alipojiinua." Mambo yote yalipokuwa salama, basi akaanza kujiinua mwenyewe, ndiposa alikuwa katika njia ya kuondoka.

31 Basi, hivyo ndivyo ilivyo, siku hizi, kwa—kwa makanisa. Imekuwa hivyo daima, ya kwamba watu wanapojisikia ya kwamba wamejitosheleza, haiwapasi kuomba tena, haiwalazimu kumngoja Mungu kwa ajili ya huduma yao.

32 Kama mtaniwia radhi kwa tamshi hili, nakubaliana na mwandishi fulani, hiyo ndiyo imesababisha wengi wa watu hawa ambao wamekuwa katika mikutano hiyo ya ufufuo wa siku hizi, ama ufufuo wa ziku za mwisho, ku—kuvurugika kabisa. Wengine wao wameona kwamba imedaiwa kuwa wamekutwa wakiwa walevi mimbarani mwao, na—na baadhi yao wamefanya makosa. Ni kwa sababu wa—wana ushawishi mkubwa sana kwa watu hata wakaanza kujisikia ya kwamba wamejitosheleza, ya kwamba huo ndio ufalme wao mdogo, nao wanaweza,

wamewashika watu sana hata wanaweza kufanya cho chote wanachotaka, nao watu hawaoni hayo. Bali Mungu huona, mwaona, huyo Ndiye. Naweza kusema...Kama Nebkadreza, siku moja, aliondoka akasema, “Tazama jinsi nimejenga ufalme mkuu,” ndiposa Malaika wa Bwana akampiga.

33 Na wakati mwanamume ama mwanamke, haidhuru yeye ni askofu ama kadinali, cho chote kile, unapoanza kujisikia ya kwamba unajitegemea, basi inakupasa kuanza kuwa mwangalifu na kujihadhari. Kwa maana, Mungu hatakuachilia kuendelea hivyo, kwa sababu Yeye hatashiriki utukufu Wake na mtu ye yote. La, bwana. Mungu ndiye atwaaye utukufu, peke Yake.

34 Wakati mwingine Mungu anaweza kumbariki mtu fulani na kumpa huduma kidogo ambayo labda ni bora kidogo kuliko ndugu zake, ama isiwe bora, bali kitu ambacho ni tofauti kidogo na ndugu zake. Punde si punde, huyo mtu huanza kujiinua, kifua mbele, na lo, jamani, angekusukuma utoke barabarani. Basi huo ndio wakati naamini mtu huyo ameanza kushika njia kutokea mlangoni, maana Mungu hawezi akatumia mtu kama huyo.

35 Huyu mfalme, ingawa alikuwa mcha Mungu, aliona amejitosheleza. Alijisikia kama angejiinua mwenyewe juu kwa kiburi, ya kwamba angechukua tu mamlaka na kufanya cho chote alichotaka, haikumpasa kuuliza mtu mwingine.

Bali, kumbuka, sisi daima tu chini ya Mungu. Mungu ni Mungu wetu.

36 Nasi twaona ya kwamba, yeye alijiinua, naye a—akajiinua sana hata akafikiri ya kwamba, kwa sababu alikuwa amekwisha ‘kubarikiwa na Mungu,’ yeye ‘angepachukua mahali pa muhudumu,’ kwa hivyo akatwaa chetezo na akaingia kupachukua mahali pa muhudumu. Yeye akaacha wajibu wake.

37 Hivyo ndivyo daima nimewaambia hawa Wafanyi Biashara wa Injili Yote, “Msijaribu kamwe kuwa wahubiri.” Wahubiri wana wakati mgumu kutosha kunyosha mambo. Ndiposa tunafanya kazi baya sana kwake na zaidi sana kuchukua mfanyi biashara ambaye hata hajaitwa kutenda hiyo kazi kamwe. Mnaona, mnapofanya hivyo, mnaruka mipaka yenu.

38 Na huenda ukapata funzo hapa. Kuna watu wengi nje, hata mimbarani usiku wa leo, wanaohubiri, ambao hawapaswi kuwa humo, kwa sababu nia yao hasa ni kujipatia riziki, ama kupendwa na watu, ama—ama kuwa na—na—na mali nyingi zaidi kuliko mtu mwingine alivyo nayo, ama kupata sifa kidogo na mtu fulani akupongeze, ama cho chote kile. Mnaona wakati mwingine wao huwa makasisi.

39 Yesu alisema, “Mnakula nyumba za wajane, na kutamani viti vya heshima, na kwa unafiki, mnasali sala ndefu.” Yeye alisema, “Ninyi mtapata tu hukumu iliyo kubwa zaidi.” Mwaona?

40 Ha—haitupasi, kamwe, kufikia mahali hapa. Hatuna budi kukumbuka daima ya kwamba Mungu anatutaka tuwe wanyenyekevu. Njia ya kupanda juu ni kushuka. Jidhili, nawe utakwezwa. Kama ukijikweza, utaaibishwa.

41 Sasa tunaona mtu huyu alijaribu kupachukua mahali pa muhudumu, naye hakuwa amestahili.

42 Walakini, Mungu alimbariki, alikuwa mtu mashuhuri. Yeye alikuwa ameuimarisha ufalme wake dhidi ya mataifa yote ya ulimwengu. Wao walikuwa wakilete utukufu na kumkabidhi yeye, kondoo na ng'ombe. Naye alikuwa na wachungaji, na wafanyi kazi wa mizabibu—bustani ya mizabibu, na, lo, kila kitu. Yeye alikuwa akiishi katika anasa, kisha akaanza kujivuna.

43 Tunaona ya kwamba hata kanisa, kanisa la mahali hapo linaweza kujidhili na kupata mahali pa—padogo kumtumikia Bwana kwa weupe wa moyo; na hebu wawe bora zaidi kidogo, mtu fulani awasaidie na wapate kanisa nzu—nzuri, ama watajaribu kulifanya bora zaidi ya lile lililoko kule chini pembeni, ndiposa washiriki watatembea barabarani kifua mbele. Hilo, mwaona, ya—yatupasa kukumbuka, hilo ni kosa.

44 Mungu aliwaambia Waisraeli, "Mlipokuwa, mimi naliwapata uwanjani, mlikuwa wakatili," na hali waliyokuwemo, "kisha mlipo lishwa, na—na kurembeshwa, halafu halafu ika . . . " wakampa Mungu kisogo, na ku- . . . ku—kufanya uzinzi, na kumwalika kila mtu kuwaona. Na tunaona ya kwamba Mungu hafurahishwi na hayo kamwe.

45 Na hata huyu mfalme mkuu na mwenye nguvu wa Isaeli hapa, alipojaribu kujifanya achukue mahali ambapo haku . . . hakukusudiwa kuchukua. Nasi tunaona ya kwamba ma—makuhani hapa, walikimbia wakamwambia, "Hapo si mahali pako. Haupaswi kufanya hivyo, kwa maana Mungu ana watu aliowaweka wakfu kwa ajili hii."

46 Jamani, laiti huduma ingalifikia mahali hapo, wale waliowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi! Kama watu wangalitambua ya kwamba kuhubiri Injili si kupata washiriki zaidi kanisani, bali ni kujitakasa kwa—kwa kusudi la kazi; tupate kuwa na watoto waliozaliwa upya katika Ufalme wa Mungu. Haidhuru wanahudhuria dhehebu gani, ama cho chote kile, ni kuwapata tu hao watoto waliozaliwa upya.

47 Kisha tunaona ya kwamba siku hizi ni vigumu sana tunapomwona muhudumu akiinuka akiwa na tukio dogo lisilo la kawaida ambalo Mungu ameweka katika huduma yake. Tunaona uigaji wa kimwili wa hilo, eti watu mbali mbali watakuja na kujaribu ku—kusema *hivi* ndivyo, wana *hili* au wajaribu jambo tofauti.

48 Namjua mtu fulani duniani siku hizi, mtu mzuri, pia, mtu mwema, mhubiri halisi wa Neno, na ni—ningesema ndu—ndugu halisi, nami nilimzungumzia si muda mrefu uliopita.

Naye akazidi kuwa na misisimuko, naye akajenga huduma yake yote juu ya msisimuko, sasa wao wanabatiza kwa Uzima wa Milele, "eti kama kwamba watu hawatakufa." Nasikitika wamejishikilia kwenye tawi ambalo hawataweza kamwe kuwa na njia ya kujitoa kwake, mwaona, basi kwa sababu hilo ni kosa.

49 "Mtu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa huzuni na taabu." Nao walio hai wanajua hawana budi kufa. Nasi tunajua, "Watu waliwekewa kufa mara moja, na baada ya kufa kuhukumu." Hivyo basi, tunajua ya kwamba ni lazima.

50 Sitaki kuishi katika nyumba hii ya magonjwa iharibikayo ambamo nimekuwa nikiishi. Inashika kila ugonjwa unaopita. Nataka moja isiyojengwa kwa mikono, iliyojengwa na Mungu, a—ambayo si mmea wa mchanganyo kama huu ulivyo. Nataka ile iliyojengwa na mikono ya Mungu, ambayo magonjwa na mauti huitoroka. Naam, wakati wo wote Yeye atakaponiita, ni—niko tayari, kwa neema ya Mungu, nikiamini ya kwamba, "Nyumba ya maskani haya iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo lingine tayari linangoja," ambalo tunaingia, ambamo hatuwezi kufa tena.

51 Ungetakaje kuishi katika huu. Si mimi. Jamani ni... Tunatoka ndani yake, nami nafurahia hilo. Na binadamu huyu wa kale, mtego wa viini tunamoishi, mtego wa mauti na kadhalika, mna kuugua na uchungu humo, na uzee. Basi kwa nini, jamani, ni nani angalitaka kuishi katika mwili kama huo? Mimi, ninafuraha kwamba kuna mmoja unaokuja. Tuna mwili ambao—ambao unatayarishwa kwa ajili yetu, Utukufuni. Na mara uhai unapokiacha hiki chombo hapa, huyo Roho wa Milele wa Mungu anayeishi humu ndani, anashika safari kwenda kwenye yale maskani kule ng'ambo, na hapo anaishi Milele. Basi, tungalitakaje kitu kama hiki? Jamani! Naam, bwana. Lo, na—nafurahi sana, ya kwamba ya kwamba kuna Mungu ambaye ameyafanya mambo haya dhahiri.

52 Na tunatazama hapa, tunaona wote ni kivuli, hata hivyo. Sisi ni kivuli. Nalitazama hapa jukwaani, nikaona mtu anayetembea, nikatazama kule barabarani nikaona wanaume na wanawake wanaotembea. Wana uhai, bali hauwezi kuwa Uhai halisi, kwa maana mna mauti ndani yake. Na—na Daudi alisema, "Nitatembea katika bonde la kivuli cha mauti." Basi, inachukua kiasi fulani cha nuru kufanya kivuli. Hapana budi pawe na nuru kiasi fulani. Kama ni giza tupu, haliwezi kufanya kivuli. Unaona? Hapana budi kuwe na kiasi fulani cha nuru, gizani, kufanya kivuli. Vema, sasa inategemea unaegemea upande gani.

53 Nikimwona mtu akitembea, kijana mwenye sura nzuri, katika miaka michache, tazama nywele zake zikigeuka kuwa mvi na kung'oka, mabega yake yanainama. Kijana mwanamke mrembo amesimama, mwenye uso wa kitawa, mcha Mungu,

akisimama na kumsifu Mungu; nami narudi katika muda wa miaka michache na kumkuta ana mabega yaliyoinama, huku amebeba watoto wawili watatu. Vema, jamani, pale, inaonyesha ya kwamba katika mwili huo mna mauti. Haidhuru ni mzuri vipi na unaonekana mrembo vipi, ungali una mauti ndani yake.

54 Basi natazama kule hiyo roho mle ndani inakoegemea. Ikiwa daima inawakilisha Nuru, inanena kuhusu Nuru, inazungumza habari za Nuru, itaambatana na Nuru. Bali kama kila mara iko upande ule mwingine, wa dunia, wa mambo ya ulimwengu, inashawishiwa na ulimwengu, hamna lingine ila kwake kuingia gizani inapokufa, kuingia katika giza la nje. Kwa hivyo unaona, tulivyo sisi, hatuna budi kukumbuka ya kwamba sisi tuko jinsi tulivyo kwa neema ya Mungu, na hamna mmoja wetu anayeweza kujivunia hayo. Tunaweza tu kuinama katika kusujudu na kwa unyenyekevu, mbele za Mungu, na kumshukuru kwa wema Wake.

55 Na tunaona ya kwamba mradi tu huyu mfalme alijisikia hivyo, Mungu alimbariki. Bali alipofikia mahali ambapo alitaka kutokudumu katika wito wake binafsi, alitaka kuchukua wito wa mtu mwingine. Naye akawaza kwa maana Mungu aliisha mbariki, ya kwamba hiyo ilikuwa sawa, angefanya hivyo.

56 Lakini ni huzuni jinsi gani tunavyofanya makosa hayo! Ni, ni vibaya jinsi gani! Ni lazima wewe, wewe uwe mwaminifu kabisa. Haikupasi, haikupasi kufanya cho chote isipokuwa Mungu amekuelekeza kwake, na kuithibitisha, na kuidhihirisha, na unajua ya kwamba ni Mungu ametenda hayo.

57 Kwa kawaida, mtu wa Mungu, Mungu hana budi kumjaribu na kumpata mtu halisi wa Mungu. Si wale watu wanaotaka mambo chungu nzima kufanya mambo kadhaa kwake, ingekuwa vigumu kwako kusema yale wangalifanya nayo kama wangaliyapata. Waona? Bali Mungu kwa kawaida hujitwalia mtu Wake, kama Musa, na Paulo, na wengineo, kumponda-ponda, kupata utukufu toka kwa maisha yake, na kumwacha awe mfungwa wa Roho Mtakatifu.

58 Sasa, tunaona ya kwamba, huyu mfalme, na jambo lingine ambalo tunajifunza hapa juu ya Uzia, kwamba, alipokanywa na mtu ambaye alikuwa na amri ya kuingiza chetezo, mtu aliyewekwa wakfu kwa ajili ya huduma hiyo. Alipomkanya, alimkasirikia.

59 Lo, li—lingekuwa jambo la laana jinsi gani! Mtu anapojaribu kumwonyesha mtu mwingine ya kwamba yu makosani, na kumthibitishia kwa Neno la Mungu, "Umakosani." Ndiposa mtu huyo kwa sababu anajisikia mwenyewe atafanya atakalo, na hatalitii Neno, basi anakasirika.

60 Umetambua yaliyompata huyo mfalme? Ukoma ukamwingilia usoni huku yu katika hasira yake. Ukoma ukampata Uzia usoni, nao makuhani na hao wengine

wakautambua, kisha wakamtupa nje ya hekalu, naye akafa, mwenye ukoma. Hayo maisha makuu yaliyoanzia vizuri sana, yaliishia kwa kuwa mwenye ukoma, na kutupwa nje, na ilimbidi kuishi katika nyumba nyingine peke yake, siku zote za maisha yake, mtu mwenye maisha ambayo wakati mmoja yalishawishiwa na Mungu.

61 Ningesema hili, kwa heshima. Tuna watu siku hizi uwanjani, vijana, na watu wenye umri wa makamu, na wazee, walioanza mbio vizuri, na wakajaribu, na wakaonyesha mienendo miema kwa Mungu. Bali tunawapata, leo, kule nje, wamelemewa na ulevi, na wamevunjika moyo, kule nje kwenye wale wengine, mbali nasi. Wengine wao walirudi nyuma, kabisa. Wengine wao wamepata wazimu wa pesa, na wengine wao wamepata wazimu wa wanawake na kuoa wanawake wengine ambao hawakuwa wake zao. Na—na mambo yote na fedheha walizopata, kila dhehebu. Sisi, mmoja hawezi kumwita yule mwingine mbaya, kwa sababu sisi sote tuna hatia, sote, ama kila dhehebu. Tumeona mtu kama huyo, ambaye wakati mmoja alishawishwa na Mungu naye alikuwa na ushawishi mwingi kwa watu. Walakini walipojisikia wamejitosheleza . . .

62 Mtu anapofikia mahali ambapo anaweza kushawishi kwa ajili ya Mungu inampasa kujidhili mwenyewe, wakati wote, daima.

63 Nasi tunaona, huyu mfalme alikufa katika aibu, mwenye ukoma. Halafu, yeye alikuwa funzo kwa huyu nabii kijana, asije akaweka tumaini lake juu ya mtu ye yote, bali amtazame Mungu peke Yake. Alipoanza kumtazama mwanadamu kama kielelezo, huyu mtu hakufaulu, ingawa alikuwa mtu mzuri.

64 Kwa hivyo ni funzo kwetu, usiku wa leo, kuweka mawazo yetu juu ya Mungu, bila kujali ni mtu gani. Hata awe kardinali, kasisi, nabii, hata awe nini, yeye si huru kutoka kwa makosa na—na kasoro, na hata mauti, na dhambi. Bali kuna Mmoja ambaye yu hivyo, na huyo ni Yesu Kristo; Yeye Ndiye tu.

Kwa hili, Isaya alijifunza somo, Mungu humwagizia mtu Wake mahali fulani.

65 Mtu hana haki kuchukua na kusema, “Vema ningepata maisha rahisi kama ningalikuwa muhudumu. Naamini nitajifunza huduma hii. Naamini nitafanya *hivi, vile* au *vinginevyo*. Naamini kama ningaliiga hiki kipawa ambacho Mungu ametoa, ingekuwa . . . Ningekuwa na mikutano mikubwa, na kadhalika.” Tunaona mengi sana ya hayo leo.

66 Bali unaona Isaya alipata funzo hapa, ya kwamba Mungu huweka mtu Wake mahali pake, Yeye Mwenyewe. Mungu ndiye huweka, Naye hakumfanya mtu huyu kuhani. Yeye alimfanya mfalme, naye anapaswa kudumu mfalme. Hapaswi ku—kujaribu . . . Isaya alijifunza hapa ya kwamba usijaribu kupachukua mahali pa mwingine.

67 Kisha alipoona ya kwamba shujaa wake mkuu alikuwa ametahayarishwa na akashuka akafa, Isaya akajisikia kwamba matumaini yote karibu yamekwisha, kwa hivyo akashuka akaenda hekaluni siku moja kuzungumza hayo na Bwana, na hapo ndipo lile ono lilipotokea. Hekaluni, akaona Yeye yule ambaye alipaswa kuwa akimwangalia wakati wote. Hekaluni, akaona, katika ono, Mungu ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana hata Mbinguni, na pindo za vazi Lake zilikuwa pamoja Naye. Hili ono aliona Kiti Chake cha enzi, kilicho juu sana, kimeinuliwa juu, juu sana ya kila milki ya duniani. Mungu, huyo Ndiye yeye alipaswa kumtazama alipokuwa katika ono.

68 Kisha tunaona hili, ya kwamba Maserafi wa Kimbinguni walikuwa wakiruka huku na huko hekaluni. Naam, Maserafi, bila shaka neno la Kiebrania hapo ni *wateketezi*. Walikuwa ndio ambao walitoa uvumba na sadaka. Ni aina ya Malaika wa hali ya juu ambao—ambao humtengenezea njia mwenye dhambi, mradi tu kuna toleo. Na hawa Maserafi, hasa, hawa *Wateketezi* walikuwa na kazi maalum, walidumu papo hapo katika Uwepo wa Mungu. Wao ni sawa na Makerubi, nao walikuwa papo hapo katika Uwepo wa Mungu.

69 Na huyu nabii aliposikia Roho ya Mungu juu yake, na akafungua macho yake. Mwaona, yeye alizaliwa kwa kusudi hilo, ya kwamba alipofungua macho yake, ilikuwa kama kushuka kutoka humu kuingia nchi fulani kama kwamba alikuwa akiota, na akaona kiti cha enzi cha Mungu kimeinuliwa juu sana. Naye akatazama hekaluni, na hawa Maserafi walikuwa wakienda huku na huko, hekaluni, wakilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu!"

70 Ni badiliko namna gani, na ilikuwa ushawishi wa namna gani juu ya huyu nabii kijana! Alipoona kuanguka kwa mtu, na ingawaje mtu mzuri angeanguka, bali sasa anamwona Mungu naye akawaona hawa Maserafi.

71 Pia tazama vifuniko maalum hawa Maserafi walikuwa navyo. Walifunika nyuso zao kwa mabawa mawili, miguu yao kwa mabawa mawili nao walikuwa wakiruka kwa mabawa mawili. Mungu kwa jumla ni mtakatifu. Wazia hilo, hata Malaika inawapasa kufunika nyuso zao takatifu, kusimama katika Uwepo wa Mungu.

72 Nashangaa, ndugu, nashangaa, dada yangu, iwapo tutachunguza hilo! Ambapo, inawapasa Malaika watakatifu kufunika nyuso zao, kusimama katika Uwepo wa Mungu, wakiwa na kicho na heshima. Bali siku hizi tunaona watu wanaojiita Wakristo, hata, hawamheshimu Mungu kabisa, ama Neno Lake, ama watu Wake, ama huduma Yake, ama cho chote kile. Watatokea wapi siku ya kiyama? Biblia inasema, "Na

mwenye haki akiokoka kwa shida, yule mwenye dhambi na asiyemcha Mungu ataonekana wapi?"

73 Na wakati, Maserafi, ile aina ya malaika wa hali ya juu sana, walio papo hapo karibu na Kiti cha Rehema, wale Wateketezaji wa sadaka, iliwabidi kufunika nyuso zao takatifu, kusimama katika Uwepo Wake, na walikuwa hapo. Na Mungu ameketi kwenye kiti Chake cha enzi, na hawa Makerubi wakienda huku na huko, wakipaza sauti, usiku na mchana "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu!" Wajua ninayomaanisha? Tazama. Wao, mabawa mawili, walifunika nyuso zao. Na ni kwa nini?

74 Tunaona siku hizi, ya kwamba, kwa maana watu wana... hawana kicho. Watakuja kanisani, watu watakuja kanisani, na—na kufanya mzaha na kucheka, kuzungumza, kutaniana, wakiketi mahali Injili inahubiriwa, hawana kicho kamwe. Nao wakutane nawe barabarani, na pamoja na...Hutazamii heshima yo yote kutoka kwa watu; haitupasi kufanya hivyo. Bali inaonyesha u—ukuu wa Kikristo angaa kuwaheshimu watu, kusema, "Salamu za asubuhi, ndugu," ama cho chote utakacho. Wengine wao hufanya "Habari zako, Mhubiri!" jamani, hayo yamekuwa kawaida sana.

75 Kumbukeni, Yesu alisema, "Mnavyowatendea hawa, mnanitendea Mimi. Yeye anipokeaye Mimi, ampokea Yeye aliyenituma. Naye ampokeaye yeye niliyemtuma, anipokea Mimi. Mnaona, mwafanyiavyo wao, mmenifanyia mimi."

76 Na utovu wa kicho, mnajua ni nini? Ni...Wao hawahisi Uwepo wa Mungu. Ulimwengu umekuwa wa—wa kawaida sana, dini imefikia kiwango cha chini sana, hata hamna heshima tena, kama tu vile imekuwa daima.

77 Watazame hao askari. Tungewazia, usiku wa leo, jinsi lilivyokuwa jambo la kijinga na la kuchukiza kwa hao askari kuweka ki—kijitambaa usoni mwa Bwana wetu Yesu, kumfanyia mzaha kwa kuwa nabii na kwamba angalijua siri za moyo. Wakaweka ki—kijitambaa usoni Mwake, na wakamweka behewani, na kuchukua kijiti na kumpiga kichwani Mwake na kisha kukipokezana wao kwa wao, wakisema, "Kama wewe ni nabii, tabiri sasa, twambie ni nani kati yetu aliyekupiga." Waona, hawana heshima kamwe. Wao hawangesikia nguvu zo zote.

78 Bali yule maskini mwanamke, mwenye imani ya kutosha ambaye ingegusa vazi Lake, yeye alipata haja zake. Mwaona, inatupasa kuwa, inatupasa kuhisi Uwepo wa Mungu.

79 Maskini hizi hisi tano tunazoishi kwazo, huo ni ulimwengu wetu mdogo. Mwaona? Bali Mungu...Hizo ni, tulipewa hizo kusudi tupate kuwasiliana na maskani yetu ya kidunia. Bali kuna hisi zilizo zaidi ya hizo, za kiwango kingine.

80 Na Mungu yumo daima. Laiti tungalikumbuka hilo. "Malaika za Bwana wamefanya kituo, wakiwazunguka wamchao." Katika jengo hili, usiku wa leo, yuasimama Yesu Kristo. Jengoni humu usiku wa leo mna majeshi ya Malaika, maelfu yao wametuzunguka. Hamuwaoni, bali mnaweza kuhisi ushawishi wao, wakiwaambieni ya kwamba wako humu. Iwapo hiyo si kweli, basi Maandiko si kweli. Na iwapo Maandiko si Kweli, basi Mungu si wa kweli. Biblia ilisema, ya kwamba, "Malaika za Mungu wamefanya kituo," hawaondoki, "wao hukaa karibu na hao wamchao."

81 Yesu alisema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa nipo hapo katikati yao." Basi hiyo inamfanya kuwa katika ulimwengu tusioweza kuuona, ambao zile hisi zetu tano haziwasiliani nao. Yesu Kristo yupo hapa. Kama tungalihisi hilo!

82 Pia, kumbukeni, si hapa tu, bali unapotembea barabarani, po pote ulipo, ninyi mnaokiri kuwa waamini na manaomcha Bwana, kumbukeni, Malaika wa Mungu wanatembea pamoja nanyi po pote mlipo. Wao wanaangalia cho chote mfanyacho, kila wazo lipitalo niani mwenu, nao wanajua habari zenu nyote. Kwa hivyo, hatuna budi kufahamu hayo.

83 Kama hatujui hayo, basi mnatenda vyo vyote. Kwa hivyo watu kwa kawaida, siku hizi, watu wengi sana, hawahisi Uwepo wa Bwana Yesu, hiyo ndiyo sababu (wao) tuna mambo haya tuliyo nayo yakiendelea sasa, yasiyo mema.

84 Kama tungalifanya vile Daudi alivyosema, "Namweka Bwana mbele yangu daima." Lo, napenda hilo. "Bwana mbele yangu daima. Aendako, namfuata. Nami najua kwamba po pote niendapo," kwa maneno mengine, Daudi alisema, "ya kwamba Bwana anaenda mbele zangu."

85 "Sitakupungukia wala sitakuacha," kasema Yesu. "Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Yeye hawezi akatuacha. Aliahidi hatafanya hivyo.

86 Hilo ndilo kusudi hasa la mikutano hii, na hilo ndilo kusudi, ndugu zangu la kuendeleza huduma yangu nje ya madhehebu, ni kujaribu kuwafanya watu waone ya kwamba Yesu Kristo yungali hai, na yuko hapa, kwa kila mwamini, kwa kila dhehebu litakalomwamini Yeye. . . ama watu katika madhehebu hayo. "Bwana yuko mbele yangu," Daudi kasema, "nami sitaondoshwa."

87 Tazama sasa, walikuwa na mabawa mawili yaliyofunika nyuso zao, kusimama katika Uwepo wa Mungu, maana hapo ndipo walipotumika.

88 Basi iwapo iliwapasa kufunika nyuso zao takatifu, kumtumikia Mungu je, muhubiri anapaswa kuwa mtu wa namna gani? Jinsi itupasavyo kufunika nyuso zetu, katika aibu! Jinsi itupasavyo kuishi! Mungu kwa jumla ni mtakatifu. Ni lazima

kwa dhamiri, kila wakati, tukumbuke hilo. Nje ya neema ya Mungu, sisi ni wenye dhambi uchi, bali Damu ya Yesu Kristo yatusafisha dhambi yote.

89 Basi walikuwa na mabawa mawili juu ya miguu yao. Hiyo inawakilisha unyenyekevu.

90 Kama Musa, Musa hakuwa mnyenyekevu sana hata alipokutana na Mungu katika kile kijiti kilichowaka moto. Bali alipoona ya kwamba huyo alikuwa Mungu kweli, na kwa sababu hii Nuru ilinena neno la ahadi. Mnafahamu? Wao walijua, na Musa alijua, ya kwamba wakati ulikuwa umewadia kwa ukombozi huu. Na hapo kinashuka chini Kiumbe cha kimbinguni, na kikarudia na kusema, "Naikumbuka ahadi yangu kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo." Naye Musa akavua viatu vyake, unyenyekevu, msingi wake wote. Yeye akavua viatu vyake.

91 Paulo, alipoona Malaika yuyo huyo wa Nuru juu yake, na kumwita "Bwana," yeye alianguka katika mavumbi ya ardhi. Akatambua. Ule unyenyekevu, "Nimekwisha!"

92 Si ajabu Isaya angelia, "Ole wangu, kwa kuwa nimemwona Bwana, Mungu wa majeshi." Huku, akiwa nabii!

93 Hata hivyo, Paulo, akiwa mtu mashuhuri, mwanachuoni, bali alipoingia katika Uwepo wa Mungu, yeye alijidhili.

94 Na Musa alipoingia Uweponi mwa Mungu, yeye alijidhili. Alikuwa nabii. Yeye alimheshimu Mungu, yule Neno.

95 Mtazameni Yohana Mpatizaji. Yohana aliposimama ukingoni, baada ya kuwabatiza watu, akatazama na kuona Nuru ile ile ikishuka kutoka Mbinguni. Akalia "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Na alipojidhili, basi Yesu akaingia majini, karibu naye.

96 Naam, hapa kuna swali niliulizwa hivi majuzi. Huenda likazuka niani mwenu. Yesu alipoingia majini, na Yohana akasema, "Ninahitaji kubatizwa Nawe basi mbona waja kwangu?"

97 Sasa maskini ndugu yangu Mbatisti, Daktari Roy Davis, alizoea kuniambia. Yeye aliniwekelea mikono aliponiweka muhudumu katika kanisa la Kimishenari la Batisti. Alisema, "Billy, kilichotendeka..." Nalimuuliza kuhusu hilo. Yeye akasema, "Ilikuwa hivi. Unaona, Yohana hakuwa ameisha batizwa kamwe, yeye mwenyewe, kwa hivyo Yesu akambatiza Yohana. Ndiposa Yohana akageuka na kufanya vivyo hivyo, kambatiza Yesu, kwa maana Yesu hangalimbatiza Yohana kabla Yeye kubatizwa." Vema, nikafikiri hilo lilisikika sawa.

98 Bali siku moja, yapata miaka miwili iliyopita, nilipokuwa nimeketi kule mwituni, Roho Mtakatifu akashuka, ile Nuru, kisha nikaona ilivyokuwa, alipoifunua.

99 Basi, hivi ndivyo ilivyo. Mnaona, pale kulikuweko watu wawili waliokuwa mashuhuri sana duniani: kulikuweko nabii Yohana; kulikuweko Yesu, aliye Masihi. Na hao, wawili, watu waliokuwa na ujumbe wa wakati huo, wakikutana uso kwa uso majini, macho yao yalipokutana. Kisha Yohana kwa unyenyekevu, akasema, "Ninahitaji kubatizwa Nawe, basi mbona Wewe waja kwangu?"

100 Yesu akasema, "Kubali hivi sasa." Hiyo ni kweli. "Bali ndivyo itupasavyo . . ." *Itupasavyo* maana yake ni "inavyofaa." Ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote." Kwa nini? Yesu akiwa Mungu; Yohana akiwa nabii. Yesu alijua upesi aliposema hayo, Yohana akiwa nabii ambaye Neno humjilia alijua yeye angelifahamu. Kwa sababu, ile sadaka, kulingana na torati, ilipaswa kuoshwa kabla haijatolewa. Na ilimpasa Yesu kubatizwa kabla hajatolewa. Yeye akasema, "Kubali hivi sasa. Hiyo ni kweli. Kwa kuwa ndivyo inavyotufaa, itupasavyo kuitimiza haki yote."

101 Lo, kama tungalichukua hayo kuwa fungu la maneno kwa dakika chache! Ya kwamba tunaona leo, kama—kama waaminio katika Nuru ya wakati ambamo tunaishi, inatupasa sisi kuitimiza haki yote. Inalipasa kanisa la Kipentekoste, kwamba tutimize haki yote, kwa kuwa tumeitwa na Roho Mtakatifu. Haitupasi kujitenga na ndugu wale wengine. Haitupasi kujiundia dhehebu na kutokuwa na uhusiano wo wote na ndugu ambaye amempokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi tulivyofanya. Haitupasi sisi. Tunapomwona Mungu akitenda kazi na kufanya mambo, na akitenda hasa yale aliyosema, na kwa sababu mtu huyo hana uhusiano na dhehebu letu, ndipo tunafanya yasiyofaa, hivyo ni vibaya. Si halali.

102 Inatupasa kuwa Wakristo. Inatupasa kuwa waungwana, Inatupasa kuwa watu wanaomcha Mungu na wanadamu pia. Inatupasa kuwa tayari kuondoka na kumsalimia kwa mkono mtu awaye yote na kuieneza blanketi upande wake kitandani, pia. Naam, kwa kuwa imetupasa kuitimiza haki yote. Sasa tunajua . . .

103 Hiyo ilikuwa kwa sababu Yeye alikuwa ile Sadaka. Naye Yohana alijua hayo, kwa maana aliona hiyo Nuru juu Yake. Naye Yohana alijidhili, akiwa mtu aliye mkuu sana hata wakati huo. Bali alipomwona huyu Bwana Yesu aliye mkuu akija, akasema, "Mimi ninahitaji kubatizwa na Wawe."

104 Lakini alipomwambia, "Inapasa kwamba tuitimize haki yote."

105 Basi Yohana akageuka, akijua, kama mtumishi wa Mungu, kama nabii, hana budi kutimiza Neno la wakati huo, kwa maana alijua ya kwamba Huyo alikuwa ndiye ile Sadaka. Alikuwa aisha sema hivyo, "Hapo yuanja Mwana-kondoo wa Mungu, yule Mwana-Kondoo wa sadaka ambaye atazichukua dhambi

za ulimwengu." Naye huyo Mwana-kondoo alipaswa kuoshwa katika birika kabla hajakabidhiwa kuhani. Amina.

106 Inatupasa kuitimiza haki yote, unapochukua Jina la Yesu Kristo. Hebu na mwanamume ye yote ama mwanamke, alichukuaye Jina la Yesu, aachane na dhambi."

107 Maungamo yetu siku hizi yameanza kuwa tu kama si—sijui nini, mafumbo ama cho chote kile. Tunashuka tunaenda na kuomba ombi la dakika mbili, na kuinuka; tunafanya kosa, nakusema, "Ee Bwana, Wewe wajua sikukusudia kufanya hivyo, bali, haleluya, mimi niko sawa," na kuendelea. La, hivyo sivyo, ndugu.

108 Inakupasa kuwa na huzuni za kiungu. Huna budi kutubu jambo hilo. Huna budi kulisahihisha. Hauwezi kutenda hivyo . . . Yesu alisema, "Unapoenda madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, uende kwake kwanza kabla hujatoa sadaka yako hapa, upatane na ndugu yako." Waona? Inatupasa, sisi, kwamba tuitimize haki yote.

109 Nanyi wanawake mlio na nywele fupi, iliyokatwa, mnajua nini? Inawapasa kuachilia nywele zenu zikue na kutenda kama bibi. Ninyi mnaovalia suruali fupi; zitoeni, mkavalie nguo. Inawapasa kutenda kama Wakristo, hiyo ni kweli, maana Biblia ilisema ya kwamba hilo ni kosa. Mwanamke hapaswi kufanya hivyo.

110 Nanyi wanaume mnaovuta sigara, hiyo haifai. Nanyi wanaume mnaowaachilia wake zenu kufanya hivyo, kisha mnasema ninyi ni "wana wa Mungu," mwanaume?

111 Ile nadhiri kuu, nadhiri kuu inayowekwa kwenye sherehe za arusi, "kupenda, kuheshimu, kutii," imekwisha. Katika nchi ya Amerika, mwanamke amechukua mahali pa kwanza. Vema, amechukua mali pa kwanza kila mahali. Biblia ilisema itakuwa hivyo kwake.

112 Wao husema ya kwamba mwanamke ndiye dereva bora sana tuliye naye nchini. Hilo ni kosa. Mimi na mwanangu tukipitia taifani, huku na kule, huwa na kitabu, na kila wakati kukiwa na kile tukiitacho kuzomewa barabarani, iwapo ni mwanamume tunakuweka upande wa mwanamume, na mwanamke chini ya mwanamke. Na katika mazomeo mia tatu kote taifani, kulikuweko na wanawake mia mbili themanini na mmoja.

113 Walifikiaje uamuzi wao? Kwa sababu ya ripoti zinazoletwa. Bila shaka, hao askari hawatawashika hao wanawake warembo iwapo wanapata nambari ya simu. Hawatawaripoti. Wanawaachilia waende, na hiyo ndiyo sababu yake.

114 Mwaona, umekuwa ulimwengu wa wanawake. Biblia ilisema ingekuwa hivyo. Bila shaka. Kwa hivyo mhubiri mimbarani yu karibu vivyo hivyo anaogopa kusema chochote dhidi yake.

115 Bali inatupasa kuitimiza haki yote. Haina budi kusemwa mahali fulani. Hautazami sifa zako na kupendwa kwako na watu wote hapa. Wewe ni—wewe ni mfungwa wa upendo wa Injili ya Yesu Kristo, na una wajibu. Wewe ni mfungwa Wake, nawe huwezi kusema jingine ila lile Roho Mtakatifu asemalo, na kuhubiri jambo lililo sahihi. Unakuwa mfungwa wa upendo Kwake. Ndipo hujali ni nini, hauna budi kuitimiza haki yote. Muhudumu anapaswa kunena hayo, ninyi watu wa Kipentekoste hasa, a—ambao mnajua ha—haiwapasi kuachilia hayo yaendelee hivyo.

116 Sasa, hapa muda fulani uliopita, mtu mashuhuri sana alinijia, kasema, "Mbona usiwaache hao wanawake peke yao?" Kasema, "Njoo hapa, nataka kukuwekea mikono na kukuombea, ili uzidi kuendelea na kuwaaombea wagonjwa." Kasema, "Naam, watu hao hukuchukua kama nabii."

Nikasema, "Mimi sikusema kamwe nilikuwa nabii."

117 Akasema, "Lakini watu wanakuchukua hivyo." Kasema, "Inakupasa kuwa ukiwafundisha watu hao jinsi ya kupata karama kubwa za kiroho."

Nikasema, "Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi."

118 Kasema, "Sikuwaambia kwamba wanakata nywele zao, na *hili, lile,* na *linginelo*. Mimi . . . " Kasema, "Inakupasa kuwa ukiwafundisha mambo makuu, mambo ya juu."

119 Nikasema, "Nawezaje kuwafundisha hesabu za herufi huku hawatajifunza ABC zao?" Hiyo ni kweli.

120 Huna budi kuanzia mahali fulani, kwa hivyo anzia chini kabisa kisha ujenge kwenda juu. Usijaribu kuanzia juu; hauna msingi wo wote. Na hiyo ndiyo shida siku hizi, ndugu zangu, wao hawachukui Hili, "Inatupasa kuitimiza haki yote."

Watazameni Malaika hawa sasa.

121 Naye Yohana Mbatizaji, Paulo, wengineo, walipouona Utukufu wa Mungu na hiyo Nuru, wao waliisujudia. Wao, naam, waliiheshimu, waliijali, kwa sababu walijidhili.

122 Pia hawa Malaika nao hata wanaohudumu Mbele Zake, hufunika miguu yao na kufunika nyuso zao. Lo, jamani! Tazama upesi sasa, Yeye alikuwa na mabawa mawili zaidi, na, kwa haya, Yeye angeanza kutenda kazi.

123 Naam, huyo ni mtumishi halisi jinsi gani, wa Mungu, alijua, anamwonyesha nabii jinsi mtumishi Wake aliyetayarishwa anavyopaswa kuwa. Je, mtumishi aliyetayarishwa anapaswa kuwa vipi? Sasa hawa watumishi hutazama . . . Yeye alikuwa amemwangalia m—mtu duniani humu na kuona jinsi alivyoshindwa, kisha Mungu akamwonyesha ufalme Mbinguni, kiti cha enzi. Huyo ndiye *Mmoja* anapaswa kuangaliwa. Kisha akamwonyesha jinsi mtumishi halisi anavyopaswa kuwa, ambaye alitumika katika Uwepo Wake. Na hapa

kulikuwepo hawa Maserafi, kisha, waliofunika nyuso zao takatifu, wakafunika miguu yao, na kwa mabawa mawili wakatenda kazi, wenye kicho, wanyenyekevu, wakitenda kazi. Amina. Iwapo huyo si mtumishi aliyevalishwa vilivyo, sijui ni nini; mwenye kicho, mnyenyekevu na anayetenda kazi. Lo, jamani! Nawaambieni!

124 Kama maskini mwanamke yule kisimani, alipoitambua ile karama ya Mungu, na huyu Mtu aliyenena alikuwa Masihi, ilimfanya aanze kazi upesi sana. Akasahau mtungi wake wa maji. Akakimbia mjini akisema, "Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyotenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye yule Masihi?" Lo, ni kitendo cha namna gani alichoingia!

125 Petro, aliposhika Neno Lake, kama tulivyokuwa tukinena asubuhi hii, kule nje mtumbwini. Je, mlitambua? Petro alipolishika Neno Lake, na kushusha ule wavu, kule ndani, na kuvua ule—ule mzigo mkubwa wa samaki, wingi wa samaki, mara Petro akaziacha zile nyavu na kuanza kazi. Kabla hajafanya hivyo, akasujudu mbele za Bwana, na kusema, "Ondoka kwangu, Ee Bwana, mimi ni mtu mwenye dhambi."

126 Kama hayo si maneno yale yale, kama, aliyosema nabii Isaya, "Ole wangu, kwa maana nimemwona Bwana Mungu, nami ni mtu mwenye midomo michafu."

127 Je! hauoni jinsi Uwepo wa Bwana unavyowafanya waaminio wa kweli? Hata hatutaki kukiri, tunataka tu kusema, "Vema, sisi ni Wapentekoste, sisi ni Wabatisti, sisi ni Wapresbeteria," na kuendelea. Lakini mtumishi wa Mungu halisi na aliyeitwa, hujidhili mwenyewe katika Uwepo wa Mungu. Yeye haulaumu.

128 Tazama waliomlaumu Bwana Yesu, walikuwa Mafarisayo, udhehebu, ndio waliomlaumu.

129 Bali mtu ambaye alikuwa tayari kuwa mtumishi Wake, alijidhili mwenyewe na kuanza kutenda kazi. Yesu alisema, "Mtanifuata, nami nitawafanya wavuvi wa watu." Alipoona ya kwamba huyo kweli alikuwa Mungu, akaanza kutenda kazi.

130 Yule kipofu aliyeponywa, Biblia ilisema ya kwamba yeye "alitangaza sifa Zake nchini kote." Yeye alianza kutenda kazi alipoona ya kwamba Mungu ana mwakilishi Wake hapa duniani, ambaye angeyafungua macho ya kipofu, na akaenda kote akitoa ushuhuda, akimsifu Mungu. Nao Mafarisayo wakamshika, na yale yangalimpata, na kama nilivyosema asubuhi hii. "Naam," yeye akasema, "siwezi kueleza, kubishana nanyi kitheologia. Bali najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona." Akaanza kutenda kazi, bila shaka, kwa maana yeye alikuwa amekwisha kutangaza sifa Zake kila mahali.

131 Na, wakati mwingine, labda wewe si muhudumu, kutangaza sifa Zake, bali maisha yako yatatangaza sifa Zake iwapo utaishi sawa hasa.

132 Maskini watu wale kule wakati wa Pentekoste, hilo kundi la wavuvi na—na watoza ushuru, na kadhalika, wenye kazi za hali ya chini. Wao walienda kule kwa ahadi ya Mungu, nao wakangoja orofani siku kumi. Na "Kwa ghafla kukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi." Nao wakaanza kutenda kazi, kwa maana walikwisha kuona ahadi ya Mungu ikidhihirishwa. Ililithibitishwa kwao, ahadi ya Mungu, na kuwafanya waanze kutenda kazi. Ahadi Yake ilipotimizwa, iliwafanya waanze kutenda kazi.

133 Rafiki, hebu niseme hili. Yale tumeona kwa mwaka mmoja au miwili iliyopita, katika Ufalme wa Mungu, yanapaswa kumfanya kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili kutenda kazi. Bali jambo ni kwamba, ha—hatuiheshimu, kufahamu ya kwamba ni Mungu. Si—sisi huwa na hamu kidogo tu. Tunapenda kuona mambo madogo, na kutupa mwamsho. Tunataka kujisikia vizuri. Tunapenda kutenda mambo haya. Bali ifikiapo kuiheshimu kwelikweli na kuiamini kwa mioyo yetu yote, inatufanya tuanze kutenda kazi.

134 Vema, yule Malaika alipokutana na Mariamu asubuhi hiyo akielekea kisimani, na akamwambia angepata "mtoto, bila kumjua mwanamume ye yote," ilimfanya aanze kutenda kazi. Akaondoka haraka, akimwambia kila mtu ya kwamba yeye angepata "mtoto, bila kumjua mwanamume ye yote." Hakujali ingemaanishaje kwa yale watu waliyosema. Yeye hakika aliisha kukutana na Malaika wa Mungu, na hiyo ikamfanya aanze kutenda kazi. Yeye alikuwa anajua ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa juu yake, akiumba uhai ndani yake.

135 Lo, laiti tungalifahamu hivyo, kwamba, Roho Mtakatifu huyo yuko juu yetu, akiumba imani ndani yetu, akijaribu kujionyesha Mwenyewe katika njia nyingi mbali mbali pamoja na vipawa, kuumba imani ya kunyakuliwa kwa Kanisa. Inapaswa kutufanya kuanza kutenda kazi. Bali nashangaa iwapo tunafanya jinsi alivyotaka iwe, kwa kicho na unyenyekevu?

136 Nguzo ya Moto katika siku hizi za mwisho inapaswa kufanya kanisa lote lianze kutenda kazi, kwa kuwa imethibitishwa, ishara za Kuja Kwake ku karibu.

137 Israeli wamerudi nchini mwao. Yesu alisema, "Mtini ukiisha kuchipuka, kizazi hiki hakitapita hata hayo yote yatakapotimia." Israeli warudipo nchini mwao na kuwa taifa, kizazi hicho kingeona kule Kuja kwa Masihi.

138 Nina habari kutoka kwa rabi fulani huko Palestina, hivi majuzi, ambazo ni za ajabu sana. Kuna mtini mdogo, mwaka huu, ambao umechipuka kule Palestina ambao haujaonekana kule kwa mamia na mamia na mamia ya

miaka. Na imebashiriwa, na Wayahudi, ya kwamba huo mtini utakapositawi tena, Masihi yuaja.

139 Wale mamajusi walioshuka kutoka Babeli, nao walikuwa wakichunguza nyota, walikuwa wenye elimu ya nyota. Na walipokuwa wakichunguza nyota, waliona hizi nyota tatu zimefanya mstari. Nyota ya Hamu, Shemu, na Yafethi, ambazo walizaliwa chini yake, zikafanya mstari, nao wakajua. Hao waamini wanasayansi walitazama sayari hizo za kimbinguni, jinsi zilivyoenda, nao walipoona hizo nyota tatu zikifanya mstari juu ya Yerusalemu. Kwa maana, kama walikuwa Babeli, walitazama moja kwa moja kuelekea Yerusalemu, kuelekea magharibi, kuziona. Nao walipoona hayo yametendeka, wao walijua ya Kwamba hizo nyota zitakapopanga mstari zenyewe, Masihi alikuwa duniani. Utukufu!

140 Na tunapoona Israeli wakienda makwao, na Roho Mtakatifu akimwagiliwa makanisani, habari za kuunganika, kwa ekumeni, na Baraza la Makanisa, na kadhalika, na Katoliki ya Kirumi ikiungana na Waprotestanti, Masihi atakuja kuchukua Bibi-arusi Wake.

141 Naye Mungu anatuma karama, kujaribu kuumba ndani yetu imani itakayotuondosha humu, hivi karibuni, katika Kunyakuliwa; kuponya wagonjwa, kuyafungua macho ya vipofu, kufufua wafu!

142 Ishara kubwa katika mbingu za juu, Malaika wakija katika kundi! Na wanasayansi wakiitazama, ilitabiriwa miezi kadha kabla haijatendeka. Ilikuwa pale. Iko pale magazetini. Ilibashiriwa miezi kadha kabla haijatendeka. Malaika saba walishuka chini na kusema, "Ufunuo mkamilifu wa siri ya Mungu ya mihuri sita ungefunuliwa. Na ikawa pale tu hasa kama Yeye alivyosema, kubashiriwa kabla haijatendeka.

143 Nao wanatazama huku na huko, wanaona namna zote za vitu vya kisiri, na kuviita namna fulani ya viumbe vya kimbinguni. Wanaviita visahani virukavyo, mambo ya kutisha mbinguni, na duniani. Ishara, ishara zinazotuonyesha ya kwamba Kuja kwa Bwana Yesu kumewadia.

144 Sasa mzabibu mdogo umechipuka. Israeli ni taifa nzima. Wana taifa lao wenyewe, bendera yao. Ile nyota ya zamani ya Daudi yenye ncha sita, bendera iliyo ya kale sana ulimwenguni, inapeperuka tena, kwa mara ya kwanza katika muda wa miaka elfu mbili mia tano. Wana jeshi lao wenyewe. Wana fedha zao wenyewe. Wako karibu. . . wamewakilishwa katika Umoja wa Mataifa. Wao ni taifa, kwa mara ya kwanza baada ya muda wa miaka elfu mbili mia tano. Nao walipokuwa wakikusanyika kule. . .

145 Nina ukanda wake, picha, tunayoiita *Usiku wa Manane Kasoro Dakika Tatu*. Na katika hiyo, wao waliwauliza hawa Wayahudi, walipokuwa wakiwaleta, wazee, migogoni mwao,

wakiwabeba. Wakasema, "Je, mlirudi makwenu mkafe? "Hasha, tumekuja kumwona Masihi." Amina. Mnapoyaona maswali hayo, hiyo ndiyo kalenda maalumu ya Mungu, ya kwamba Masihi yu ajiandaa kutokea. Lo, jamani!

146 Jinsi inatupasa kuwa wanyenyekevu. Jinsi itupasavyo kuwa na kicho. Jinsi itupasvyo kuwa tukitenda kazi, tukijaribu tuwezavyo kuifanya kila nafsi iokolewe, tukisambaza mbegu kulia hata kushoto, na kufanya kila tuwezalo.

147 Bali badala ya hayo, tunasema, "Mungu atukuzwe, sijisikii kama kwenda usiku wa leo. Naamini, vema, naamini nitakaa nyumbani na kuona kipindi hiki kizuri cha televisheni usiku wa leo. Ni mkutano wa maombi, bali . . . " Kanisa linalolala, la Laodikia, tajiri! Lo, jamani! Tuko hapo.

Inapaswa kutufanya tutende kazi.

148 Sisi kama yule nabii, tumeona tukitoka kujikweza wenyewe madhehebuni. Tunaona hasa siku hizi, kanisani, mambo ambayo yalitendeka, kama Isaya alivyoona. Aliona mtu ambaye ingawa aliheshimiwa na Mungu, bali tulimwona, alimwona akijikweza kisha akapigwa kwa ukoma. Sisi leo, tunaona jambo lile lile, la madhehebu yaliyojikweza yenyewe. "Sisi ndio wakubwa sana kati ya kundi hilo. Tuna wafuasi wengi kuliko wengine wote." Kujikweza wenyewe, twaona ukoma wa kutokuamini ukiwapiga, nao wanatupwa nje.

149 Ndipo inatupasa tuwe tumetazamia ono kutoka Mbinguni, ambalo litamwonyesha Yesu Kristo miongoni mwetu. Neno Lake la ahadi ya kwamba Yeye atafanya hivyo, naam, bwana, bila kushawishiwa na mipango iliyobuniwa na binadamu, bali kushawishiwa na Mungu Mwenyewe.

150 Tunawaona wao, kama Uzia, wakiachilia Neno, kwa maana wamelibadili na kanuni za imani, wakijaribu kujifanya wenyewe kama Uzia wa kale, wakijaribu kuchukua mahali pa huduma iliyo na upako nyuma ya jukwaa, na kukataa lile Neno la kweli la Mungu. Hawana shughuli huko kuliko Uzia alivyokuwa nayo huko kwenye hayo madhabahu, pamoja na uvumba. Mtu anayedai kuwa Mkristo, na atakana hakika za Neno, hana shughuli mimbarani kuliko alivyokuwa Uzia na kile—na kile chetezo. Mtu aliyedai kubatizwa na Roho Mtakatifu, na akabarikiwa na Mungu, na atasimama na kukana hiyo Biblia na Kweli Zake, amekwisha kuibadilisha na kanuni fulani za imani ama kitu fulani, amejaa ukoma wa dhambi na kutokuamini kama Uzia alivyokuwa.

151 Yeye aliondolewa kwenye hiyo huduma, bali wao hujaribu kutimiza hiyo hudumu kwa elimu zao, "Mimi ni Daktari Ph.D, L.L.D. *Fulani*. Waona, wao hujaribu kuchukua hiyo na kudai elimu badala ya upako Roho Mtakatifu. Mnaona, basi, mtu anaweza akachukua hiyo Biblia, na vyuo vinaweza kuifafanua na kuitenganisha, na kuiweka kule nje na kuiunganisha tena

kuifanya ionekane nzuri sana kwako. Hiyo ni elimu. Hiyo ni kwa sababu ameisoma na kuisoma, pembe zote na kadhalika, jinsi ya kuiunganisha.

152 Bali hebu niwaambieni jambo fulani. Mungu anaposhuka katika Neno Lake, Yeye haliunganishi tu, Yeye hulidhihirisha kule na kulifanya hai, na kulithibitisha na kulishuhudia, ya kwamba ni Kweli. Huo ndio Ukweli wa Neno. Hapo ni wakati Mungu Mwenyewe anaposema.

153 Hilo ono lilimgusa moyo huyo nabii. Lo, jinsi hilo ono lilivyokuwa na matokeo kwake. Lilimfanya huyu nabii . . .

154 Sasa, kumbukeni, alikuwa akimtazama binadamu. Bali alipoona jambo halisi . . . Aliyatazama maisha matakatifu ya mwanadamu, akamwona akikosea, akamwona akiambukizwa ukoma kisha akafa. Mnatazama jambo lile lile katika madhehebu yenu. Mmeona mahali kila mojawapo limekwenda?

155 Sasa huu mwenendo mkuu wa ekumeni. Kama kanisa halimo katika mwenendo huu wa ekumeni, wakati wa—wa hatari, kanisa hilo haliwezi kutumiwa kama kanisa. "Na hamna muhudumu anayeweza kumhudumia mtu ye yote, atauawa kwa kufanya hivyo. Kama akihudumu baraka kwa watu walio nje, yeye yuko pamoja na mwenendo wa ekumeni." Hivyo ndivyo hasa imeandikwa leo, na Mlutheri; nimesahau jina lake. Mwaona, hiyo ni kweli." Kanisa lenu haliwezi kuabudiwa; litafanywa ghala." Mwaona ile alama ya mnyama ikianza kutenda kazi, nasi tunaitazama. Wakati, lo, unapaswa kuliingiza kanisa katika kitendo. Bila shaka, unapaswa kufanya hivyo.

156 Tazameni matokeo ya hilo ono sasa, liliyomfanyia huyo nabii. Lilimfanya . . . baada ya kumtazama huyo mtu, na kuona akikosea. Aliona Mungu akimkasirikia huyo mtu, na kumwacha, na kumpiga kwa ukoma.

157 Kisha akashuka kwenda hekaluni, kusema, "Bwana Mungu, najua Wewe u Mungu. Na nimekuwa nikitazama kitu kilicho makosa." Halafu Mungu akamwonyesha ono. Na si ono peke yake, bali hilo ono lilithibitishwa; kwa maana huko katikati kulikuweko Maserafi wakiruka huku na huko, na hata sauti zao zikalitikisa lile jengo zilipoungana, visingiti vyake.

158 Ndiposa waona aliona jambo halisi. Na bado, yeye alikuwa nabii. Yeye alikuwa . . . Na—nabii ndiye anayejiliwa na Neno. Bali alikuwa hajafikia kiwango kilicho zaidi ya yale aliyokuwa akiangalia, kwa shujaa wake, Uzia, akimwangalia mchungaji wake, yu—yule mtu mashuhuri. Na alipoona mkosaji pale, wa Neno, na akaona hilo Neno likimkemea huyo mtu kwa sababu alikuwa akitwaa afisi ambayo haikumhusu kwa vyo vyote, basi nini ilitendeka? Akainua macho yake, naye akamwona Bwana.

159 Je, mnaweza kusoma katikati ya mistari? Mnaweza kuona ninayosema sasa? Bwana Yesu aliyeahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana

wa Adamu." Mungu yule yule aliyeandika Biblia, kasema, "Yesu Kristo ndiye yule jana, leo, na hata milele." Naye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya." Mnafahamu ninayomaanisha?

160 Kisha huyo mtu mwenye moyo mwaminifu akaona Utukufu wa Mungu, akauona kwa vitendo. Naye akalia kwa sauti kuu, kama mwenye dhambi, na kukiri ya kwamba yeye ni mwenye dhambi. Yeye alikuwa hajapata kamwe kuona kitu kama hicho, dhahiri sana, hapo mbeleni. Alikiri ya kwamba yeye alikuwa mwenye dhambi.

161 Kisha kukatendeka nini? Wakati huyo nabii alipokuwa tayari kukiri, ndipo kutakaswa halisi kukaja.

162 Hata watu watakapokuwa tayari kukiri, hamna haja ya kuwa na hizi ibada za uponyaji. Kama utakiri dhambi zako, ukiri kutokuamini kwako, ukiri mambo unayotenda makosa, basi Mungu anaweza kutenda kitu fulani. Bali hata kutakapokuwa na kutubu, hakuwezi kuwa na utakaso.

163 Na mara Isaya aliposema, "Ole wangu! Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami naishi pamoja na watu wenye midomo michafu." Ndipo kukaja maungamo, hayo, kisha wakaja Maserafi na Moto. Umeona? Mungu hakutumia kamwe seminari kumtakasa kwayo. Hakutumia kamwe ki—kitabu cha torati kumtakasa kwake. Yeye alimtakasa kwa Moto.

164 Mungu daima hutakasa watumishi Wake, anapokuwa tayari kuwaweka katika huduma, kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Mungu hutakasa kwa Moto; si kwa vitabu, si kwa elimu, si kwa mawazo ya kielimu, si kwa dhehebu. Bali kwa Moto wa Roho Mtakatifu, Mungu hutakasa mtumishi Wake.

165 Ndipo tazama, basi, baada ya maungamo, baada ya utakaso, ndipo likaja agizo. Kisha kulikuweko na agizo. Baada ya kuungama na kutakaswa, ndipo Isaya aliyetakaswa alipomjibu Mungu, na kusema, "Mimi hapa, nitume mimi." Akiisha kutakaswa, kuungama, kutakaswa kwa ule Moto, ndipo Isaya aliyetakaswa akawa tayari kwa huduma. Yeye alikuwa tayari kuwa mfano. Alikuwa tayari ku—kutoa maisha yake, kusudi wengine wapate kushawishika kwayo.

166 Lakini hadi alipoungama hayo, hadi alipotakaswa, basi alikuwa ushawishi mbaya, kibaraka tu wa huyo mfalme.

167 Sasa yeye ameisha takaswa, sasa ameungama na kutakaswa, na kuitwa na kuagizwa kuwa nabii. Naye Mungu akamruhusu kuandika Biblia nzima, katika Vitabu sitini na sita vya Biblia, mna sura sitini na sita za Isaya. Yeye anaanza katika Mwanzo; katikati ya kitabu ni Yohana Mbatizaji; naye anaenda moja kwa moja hata kwenye ule utawala wa Miaka Elfu, katika Isaya 65 na 66, hiyo ni kweli, Ufunuo. Yeye aliandika Biblia nzima kwa muhtasari. Kwa nini? Kwa sababu yeye alijidhili alipouona Uwepo wa Mungu.

168 Je, yeye alifanya nini? Naye, baada ya kufanya hayo, na kujidhili na akatakaswa na kuwekwa wakfu, na kutakaswa na kuagizwa, yeye ameisha kuwashawishi mamilioni ya watu. Kiko hapa Kitabu Chake, Maandiko ya Isaya yako hapa ambayo yamewashawishi wanadamu tangu wakati huo hadi wa leo. Ushawishi wake unaendelea.

169 Biblia ilisema, "Kazi zao zinawafuata." Kama vile Roho Mtakatifu alivyomwambia Yohana, katika Ufunuo, ama kwenye Kisiwa cha Patimo, "Imekupasa kutoa unabii bado juu ya wafalme na mataifa na watu." Kitabu cha Ufunuo kingali kinatoa unabii. "Wanapumzika baada ya taabu zao, bali matendo yao yafuatana nao." Ule ushawishi waliokuwa nao, ungali unawafuata. Mwaona? Bila shaka, ndivyo ilivyo.

170 Na sasa, leo, tunaona jambo lile lile, ushawishi. Hatuna budi kushawishi.

171 Kabla hatujashawishi, hatuna budi kumtambua Mungu, hatuna budi kutakaswa, hatuna budi kuwa wanyenyekevu. Inatupasa kujishusha, na kujua, tukiendelea kuwazia na kujua jinsi mlivyo wadogo. Wewe si kitu. Mimi si kitu. Na hamna ye yote wetu aliye kitu, bali Yeye ni vyote. Yeye anastahili sifa zote, Ee, Mwana-Kondoo wa Mungu. Tunachohitaji ni kurudi hekaluni, tunahitaji kurudi madhabahuni mwa Mungu na kutengeneza madhabahu mioyoni mwetu, ambapo tunaweza kujisalimisha wenyewe, kisha tumwone Bwana Mungu wa majeshi akishuka chini katika hizi siku za mwisho na kutenda aliyotenda alipokuwa hapa kwanza. Ndipo utafahamu, na kulia, "Ole wangu!"

> Kaa la Moto lilipomgusa nabii,
> Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo kuwa
> Sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, Bwana, hapa, nitume mimi."

172 Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu na tuuimbe.

> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nita . . . kujibu upesi;
> Nena, Bwana wangu, nena Bwana wangu,
> Nena, nami nitakujibu, "Bwana, nitume mimi."

Sikizeni, marafiki.

> Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu;
> Sikizeni kilio chao cha huzuni na uchungu;
> Hima, ndugu, kimbia ukawaokoe;
> Jibu upesi, "Bwana, mimi hapa."

Sasa nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu upesi;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

173 Je, mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kwa muda mchache tu, tukivumisha huu. [Ndugu Branham anaanza kugugumiza, kisha anaanza kuimba.]

Kaa la Moto lilipomgusa nabii,

174 Hebuni na tuuvumishe sasa. [Kusanyiko linagugumiza huku Ndugu Branham anapoendelea kuimba—Mh.]

Likimfanya msafi kama usafi uwezavyo kuwa,
Sauti ya Mungu iliposema, “Tumtume nani?”
Ndipo nikajabu, “Bwana, hapa, nitume.”

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakujibu upesi;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nani nitakujibu, “Bwana, nitume mimi.”

175 Baba wa Mbinguni, tunangoja kusafishwa kutokuamini kwote, kwa maana hakika mamilioni wanakufa sasa katika dhambi na aibu. Itatufaidi nini, Bwana, kwamba sisi—kwamba tukiri, bila kuwa na kile tunachodai kuwa nacho? Inatufaidi nini kujaribu kuwazia kwa akili zetu ya kwamba jambo fulani limetendeka, huku tukijua kweli halijatendeka? Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba utatutakasa sasa kutoka kutokuamini kwote, na mambo yetu yote ya maisha ya kimwili, tukapate kusafishwa na Damu ya Bwana Yesu.

176 Kundi hili hapa Chicago, kwa ono asubuhi iliyopita, Bwana, najua kuna sehemu moja ya Bibi-arusi inayongoja hapa, nami sijui jinsi ya kuipata, Bwana. Mimi ninapanda mbegu tu po pote niwezapo. Naomba, Mungu, iwapo kunao hapa, usiku wa leo ambao—ambao hawana—hawana kituko hiki, ambao kamwe hawajakuwemo na kuona Ufalme halisi wa Mungu ukidhihirishwa, hawajaona matokeo yake, na kuona maisha yao yakiambatana na Neno lote, na wanaweza, na kadhalika; Bwana, tujalie usiku wa leo ya kwamba huu utakuwa usiku ambao watafanya hivyo. Tujalie, Baba. Tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

177 Sasa kwa kicho. Ni—nina hakika mnanijua vyema kutosha, ama natumaini mnanijua. Mimi si mshupavu wa dini. Iwapo ndivyo nilivyo, si—sijui. Siamini ya kwamba Mungu huwaheshimu washupavu wa dini. Miaka hii yote, na kote uwanjani, kungekuwa na kutendeka kwa jambo fulani. Mimi ni ndugu yenu. Bali na—naamini kwa moyo wangu wote ya kwamba. . .Naam, siwezi kusema ya kwamba Bwana aliniambia, bali naamini ya kwamba kizazi hiki kinachoishi sasa kitashuhudia kule Kunyakuliwa. Hivyo ndivyo kulivyo karibu,

naamini. Siwezi kuona jambo jingine linalokuja. Mnaona, kila kitu kimekwisha kuingia mahali pake.

178 Mnakumbuka jambo la mwisho lililotendeka kabla Sodoma haijateketezwa? Bwana alidhihirishwa katika mwili wa binadamu. Naam, Yeye alikuwa binadamu. Alikula nyama na akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na akala mkate wa mahindi, na akala ndama wa ng'ombe, na akasimama pale na akala. Hata hivyo Ibrahimu, aliyenena Naye, alisema alikuwa "Mwenyezi Mungu." Katika mwili wa binadamu? Naam. Yeye alikuwa akionyesha kwa mfano yale atakayofanya katika siku za mwisho. Yesu alitaja hayo.

179 Na tazama huduma aliyoitenda. Jambo la kwanza, Yeye alirejea kwa ahadi Yake. Aa! Unaona sehemu yake ya theologia? Waona, Yeye alisema, "Nalikufanyia ahadi, na sasa niko hapa kuiimarisha." Na sasa tunajuaje hiyo ahadi ni. . . Tazama hiyo. Wao walikuwa wakingoja. Kabla tu ule moto haujashuka, Ibrahimu na Sara walikuwa wakingoja yule mwana aliyeahidiwa. Mungu akaonekana katika mwili wa binadamu na akafanya ishara mbele zao, ambazo Yesu alisema zingekuwa vile vile katika Kuja Kwake, ya kwamba Yeye ndiye Mwana aliyeahidiwa. Na tumeona hayo kwa sasa, yakiendelea, miaka kumi na mitano.

180 Na hata hivyo kanisa linaendelea kuwa baya zaidi. Si ajabu, tunaweza kuona kweli ya kwamba tuko katika Wakati wa Laodikia.

181 Sasa Roho Mtakatifu yuko hapa. Huenda kuna wengine hapa. . . Tuna, tuna, tuna, tu—tumekuwa tukiwaombea wagonjwa bali ninatoa wito wa madhabahuni. Ninafanya mwito wa madhabahuni kwa wale wanaoungama pamoja na wale ambao hawajaungama. Nawaulizeni ninyi mwandamane nami hata hekaluni mwa Mungu, ambalo limo ndani yenu. Nendeni katika kibanda cha maungano mioyoni mwenu, mkaseme, "Bwana Mungu, nitakase. Na umtume yule Malaika, mwenye kaa la Moto, a—aondoe kwangu kutokuamini kwote, kusudi usiku huu nipate kutambua Uwepo wa Mungu, kama nabii Isaya alivyofanya yule Malaika alipomgusa." Nawatakeni mfanye hivyo, na muwe waaminifu kabisa.

182 Na sasa tuna ahadi ya wakati huu. Hatujaahidiwa theologia chungu nzima. Tumeahidiwa . . .

183 Tazama, Wa—Waebrania walikuwa na miaka elfu mbili ya theologia, bali walipewa ishara fulani. Kabla hawajaangamizwa. Lutu na wengineo walikuwa wamepewa ishara nyingine. Wao waliona ishara ile ile. Na sasa kama Mungu akiwaachilia watu . . . Yesu alipokuwa hapa, Yeye alifanya ishara ile ile kwa Waebrania, na akawafanyia Wasamaria, wala si kwa Mataifa.

184 Basi huu ni mwisho wa Wakati wa Mataifa, kama ilivyokuwa wakati huo kwa wakati wao. Kanisa la Kimataifa tayari linaitwa. Naam, Mungu hawezi akabadili mpango Wake, kwa sababu Yeye hana kikomo, naye ni mkamilifu, yuko mahali pote, anajua yote, ana nguvu zote, wala hana kikomo. Kama sivyo alivyo, Yeye si Mungu. Kwa hivyo, unaona, hana budi kufanya jambo lile lile alilofanya wakati huo. Hiyo ndiyo sababu wao walijua katika kila kizazi ya kwamba Yeye hujidhihirisha Mwenyewe, alikuwa vivyo hivyo, wakijua kwamba ni yeye yule.

185 Naam, Yesu Kristo angalisimama hapa, usiku wa leo, kwenye hili jukwaa; kama angalisimama hapa, jambo pekee ambalo angalitenda, lingekuwa jambo lile lile alilotenda alipokuwa hapa, kuwafanya watu wafahamu ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu.

186 Sasa Yeye yuko hapa. Aliahidi atakuwa hapa, na sasa njia pekee anayoweza kutenda kazi ni kwa ahadi Yake. "Mimi ndimi mzabibu; ninyi ni matawi." Na matawi hushuhudia ya kwamba uhai unatoka kwa mzabibu, ama hayana uhai wo wote ndani yake. Bali yanatiwa nguvu na huo uhai, yana uhai ule ule mzabibu ulio nao. Una—unajishurutisha, au unajisukumiza kuingia katika tawi.

187 Sasa iweni na kicho kwa muda mchache. Na Mungu wa Mbinguni anisaidie, hata, ninyi niliowahubiria katika hubiri hili, ambao wakati . . . Isaya, Yule mwamini, alipofikia mahali alipoona makosa ya huyo mtu aliyejaribu kumwakilisha Mungu, kisha akaona Mungu akishuka chini, na ikawa kweli, ndipo akalia, "Ole wangu!" Kwa maana, Mungu alikuwa amefanya ahadi hivyo. Aliifanya kwa kila kizazi. Yeye anatufanyia sisi, katika kizazi hiki chetu. Tunaona kila kitu kikiwa katika utaratibu kwa ajili ya Kuja Kwake.

188 Basi, je, mnaamini Yeye yuko hapa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi na anisaidie.

189 Nataka kujua ni watu wangapi wagonjwa walio hapo, inueni mikono yenu. Iweni na imani. Na sasa nawaulizeni kuchukua Andiko hili, Waebrania, ya kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungano yetu, naye anaweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu."

190 Basi omba, "Mungu, hebu nikuguse Wewe. Ndiposa nawe, kwa ajili hiyo, unene kupitia kwa Ndugu Branham, kama ulivyofanya kupitia kwa Mwanao halisi. Yeye ni mtoto aliyefanywa mwana, kama nilivyo mimi. Bali Wewe umeahidi ya kwamba katika hizi siku za mwisho utafanya hivyo. Sasa, Bwana, hebu nione jambo lililo halisi." Nawe uombe.

191 Na Mungu wa Mbinguni, kulingana na jinsi moyo wangu ulivyotolewa kwa Chicago na po pote niendapo, na Yeye athibitishe hayo kuwa hivyo.

192 Huyo mtu ambaye aliinuka kitini mwake, yeye ni mtu mkubwa, anayeketi papa hapa mbele yangu hapa, ameinua mikono yake juu. La, huyo aliye hapo nyuma, amevalia shati nyeupe. Si wewe mwenyewe hasa, bali unamwombea mtu mwingine. Ni muhudumu. Je, unaamini naweza kukwamba shida yake? Yuna ugonjwa wa moyo. Ikiwa hiyo ni kweli, punga mkono wako. Amini kwa ajili yake.

193 Ukiamini tu! Bali huna budi kuamini. Kama huamini, haitakufaa kitu. Mtu huyo ni mnyenyekevu.

194 Hapa, hapa, hapa yuaketi mwanamke ameketi papa hapa chini upande huu, mwanamke wa pili katika safu ya pili hapa, papa hapa. Yeye yuna ugonjwa wa chango. Ameambukizwa changoni. Maskini mwanamke yule kule mwisho, aliye na mvi, simama kwa miguu yako kusudi watu wapate kukuona. Naam, ni wewe. Hiyo ni kweli. Umeambukizwa changoni, na pia una kasoro zingine, shida zingine, shida nyingi. Kama hayo ni kweli, inua mkono wako.

195 Naam, yeye aimgusa nani? Si mimi. Alimgusa Yeye. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

196 Hapa kuna bibi anayeketi papa hapa nyuma. Yeye yuna shida, mvumo kichwani mwake, wasiwasi, shida nyingi. Bibi Pfeiffer, amini kwa moyo wako wote, simama kwa miguu yako. Sikujui, bali Yesu Kristo anakupa mahitaji yako. Sijamwona maishani mwangu; yeye ni mgeni kwangu. Itakwisha. Usifadhaike. Imani yako ilikuponya.

197 Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, Amina—Mh.] Hamwoni hayo ndiyo aliyoahidi?

198 Huyo mtu anayeketi kule nyuma. Hapo, je, hamuioni ile Nuru? Ni mgonjwa sana. Yeye yuna tezi kooni mwake. Amekwisha kufanyiwa upasuaji; daktari hakumpa matumaini kwake. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Je, unaukubali, Bw. Stonelake? Je, unaamini kwa moyo wako wote? Vema, simama kwa miguu yako, Yesu Kristo atakupa afya.

"Ukiweza kuamini!"

199 Huyu mwanamke humu kwenye haya machela. Hapana shaka, huna kadi ya maombi, hamna kitu kama hicho sasa. Wewe umepooza. Je, unaamini hii kuwa Kweli? Je, unaamini ya kwamba uliyosikia usiku wa leo ni Kweli? Ukikaa pale, utakufa. Bali Yesu anaweza kumponya mtu aliyepooza. Je, unaamini atafanya hivyo? Kama utaamini hilo na kulikubali, basi unaweza kuinuka na kutoka kwenye kitanda hicho na kwenda nyumbani, katika Jina la Yesu Kristo, na kupata afya.

200 Huyo! Yu aja pale akiinuka toka kwake. Mtu fulani amsaidie kuinuka kidogo pale yeye amepooza. Mtu fulani. . .Anakuja pale peke yake, ametoka kitini, ameponywa, katika Jina la Yesu Kristo.

201 Je, mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linafurahi—Mh.] Basi simameni kwa miguu yenu na . . .

202 Anakuja pale yule mwanamke aliyepooza akitembea katikati ya wasikizaji! . . .?. . .

Nena, Bwana wangu, paka mafuta.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Makutano wanafurahia—Mh.]

203 Hapa kuna mtu mwingine, mmoja alikuwa amepooza, kutoka kitandani; akatoka kitandani, akimsifu Mungu.

Mnaamini? [Makutano wanafurahi—Mh.]

204 Yuko wapi mwingine, machela yote ni matupu, kila kitu! Kila mtu amesimama, wakimsifu Mungu!

Kaa la Moto lilipomgusa nabii!

205 Huyo hapo mwanamke aliyepooza akitembea jukwaani! Mungu asifiwe! Mpeni utukufu na sifa!

206 Hapa kuna mtu mwingine akija jukwaani. Mwangalieni akipanda vipandio, Ndugu Fitch.

207 Na tumpe Mungu sifa. Inueni mikono yenu mkampe Mungu utukufu. [Kusanyiko linaendelea kumsifu Mungu—Mh.]

*USHAWISHI* SWA63-0803E
(Influence)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, Agosti 3, 1963, kwenye mkutano wa Chama cha Wafanyi Biashara wa Injili Yote katika ukumbi wa Shule ya Upili ya Ufundi ya Lane kule Chicago, Illinois, Marekani umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org